



CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI DODOMA – TANZANIA

S.L.P. 138
DODOMA
Tanzania

Toleo Na 56

Simu: +255 262963037
Nukushi: +255 262963036
Barua Pepe: mpro@irdp.ac.tz

Tovuti: www.irdp.ac.tz

TAARIFA KWA UMMA

UTEUZI

**BIBI. CAROLINE G. NGEREZA ATEULIWA KUWA KAIMU MKUU WA MASUALA
YA MIPANGO, FEDHA NA UTAWALA WA KITUO CHA MAFUNZO CHA KANDA
YA ZIWA - MWANZA**

Dodoma, Jumatano 30 Machi, 2022.



Bibi. Caroline G. Ngereza

Ndugu wanajumuiya wa Chuo Cha Mipango ya Maendeleo Vijijini na umma wa wataanzania kwa ujumla mnataarifiwa kuwa Mkuu wa Chuo Cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Prof. Hozen K. Mayaya amemteua Bibi. Caroline G. Ngereza kuwa Kaimu Mkuu wa Masuala ya Mipango, Fedha na Utawala wa Chuo Cha Mipango Kituo cha Mafunzo kanda ya Ziwa – Mwanza.

Bibi. Caroline G. Ngereza alijiunga na Chuo Cha Mipango mwaka 2009 ambapo kwa kipindi chote hicho amepata uzoefu wa kutosha wa uongozi na utawala kutokana na kushika nafasi mbalimbali za uongozi. Baadhi ya nafasi hizo ni pamoja na Mratibu wa Udahili na Mitihani wa Kituo cha Mafunzo Kanda ya Ziwa; Mthibiti Ubora wa Taaluma wa Kituo cha Mafunzo Kanda ya Ziwa; na Mratibu wa Masomo ya Uzamili nafasi aliyokuwa anaishikiria kabla ya uteuzi huu ulioanza tarehe 04 Machi, 2022.

Bibi. Caroline G. Ngereze ni Mtakwimu ana Shahada ya Umahiri ya Takwimu (Masters of Arts in Statistics) na Shahada ya Kwanza ya Takwimu (Bachelor of Arts in Statistics) kutoka Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. Kwa sasa amekamilisha masomo yake ya Shahada ya Uzamivu(PhD) katika Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam na anategemea kuhitimu mwaka huu 2022.

Imetolewa na,

Godrick H.B. Ngolly
Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Uhusiano